

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 7 WA WANAHISA WA MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

7.1 Taarifa inatolewa kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 7 wa Mwalimu Commercial Bank Plc utafanyika katika Ukumbi wa **MABELE HALL - MABEYO COMPLEX Dodoma, siku ya Alhamisi tarehe 24 Agosti 2023 kuanzia saa 5:00 Asubuhi.**

7.2 Ajenda ni kama ifuatavyo:

7.2.1 Kufungua Mkutano.

7.2.2 Kuthibitisha Taarifa na Akidi

7.2.3 Kupitisha Ajenda.

7.2.4 Azimio la Mgongano wa Maslahi.

7.2.5 Uthibitisho wa Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 6 wa Mwaka 2022.

7.2.6 Kujadili yatokanayo kwenye Mkutano Mkuu wa 6 wa Mwaka 2022.

7.2.7 Taarifa ya Mwenyekiti.

7.2.8 Kupokea Ripoti ya Wakurugenzi na kupitisha taarifa za Hesabu za Fedha za Mwaka 2022.

7.2.9 Azimio la Gawio .

7.2.10 Hatua iliyofikiwa katika kuongeza mtaji.

7.2.11 Kupokea na kuidhinisha Malipo ya Wakurugenzi.

7.2.12 Kupokea na kuthibitisha Uteuzi wa Mkaguzi wa nje.

7.2.13 Kuwaongezea muda Wakurugenzi waliomaliza muda.

7.2.14 Mengineyo yatokanayo na Mkutano.

7.2.15 Tarehe ya Mkutano ujao.

7.2.16 Kufungwa kwa Mkutano.

7.3 Mwanahisa yeyote ambaye anataka kuingiza pendekezo lake katika kipengele cha 7.2.14 hapo juu lazima atoe taarifa kwa maandishi siku tatu (3) kabla ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.

7.4 Mwanahisa atakayeshindwa kuhudhuria, ana haki ya kuteua mwakilishi kuhudhuria mkutano kwa niaba yake. Taarifa hizi zimfikie Katibu angalau saa arobaini na nane (48) kabla ya wakati wa mkutano.

Fomu za mwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya Mwalimu bank (www.mwalimubank.co.tz).

7.5 Wanahisa wote wanaombwa kuja na vyeti vya hisa pamoja na vitambulisho siku ya mkutano.

7.6 Makabrasha ya mkutano yanapatikana kwenye matawi yetu ya Samora Avenue na Mlimani Tower

Dar es Salaam; katika ofisi zetu wakilishi za kanda na kwenye tovuti ya Mwalimu bank

(www.mwalimubank.co.tz). Pia yatapatikana kwenye ukumbi siku ya mkutano.

7.7 Gharama za usafiri na malazi zitafanywa na wanahisa wenyewe.

Mwalimu Commercial Bank Plc

TAARIFA hii imepokelewa na kuthibitisha uwepo wa akidi ya wanahisa mahususi wa mkutano huu kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Benki.

TAARIFA YA SEMINA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kuwa, kutakuwa na semina kwa wanahisa katika Ukumbi wa **MABELE HALL- MABEYO COMPLEX Dodoma, siku ya Alhamisi tarehe 24 Agosti 2023 kuanzia saa 3:00 Asubuhi.**